# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

DAR ES SALAAM & KILIMANJARO



# JARIDA LA MTANDAONI

OKTOBA - DESEMBA, 2025



Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo Fedha, Utawala na Mipango Dkt. Eventus Mugyabuso (mwenye suti wa pili kushoto) akikabidhiwa Juzuu za Maamuzi ya Migogoro ya Kazi na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Tanzania Divisheni ya Kazi, Dkt. Y. J. Mlyambina (mwenye suti ya bluu kulia), Oktoba 2025.

## MAKABIDHIANO YA JUZUU ZA MAAMUZI YA MIGOGORO YA KAZI KWA CHUO CHA USTAWI WA JAMII (ISW)

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania – Divisheni ya Kazi, Dkt. Y. J. Mlyambina, tarehe 10 Oktoba 2025, amekabidhi Juzuu za Maamuzi ya Migogoro ya Kazi kwa Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), zikiwemo nakala mbili (2) za Juzuu za Mahakama Kuu na nakala sabini (70) za Labour Court Case Digest.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Dkt. Mlyambina amesema kuwa hatua hiyo ilikuwa ni kutambua mchango wa ISW kama chuo pekee nchini kinachotoa taaluma za kazi na kuandaa wataalamu wanaohudumia Mahakama za Kazi. Kwa upande wake, aliyekuwa Kaimu Naibu Mkuu wa Chuo – Fedha, Utawala na Mipango, Dkt. Eventus Mugyabuso, amemshukuru kwa mchango huo akieleza kuwa Juzuu hizo zitakuwa rejea muhimu na zitaongeza ujuzi kwa wanafunzi na wanazuoni wa taaluma za kazi.



Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii Dkt. Joyce Nyoni (Kushoto) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa One Tanzanite Football Academy Agapiti Emmanuel (kulia) wakionesha hati za makubaliano, Novemba 2025

# UTIAJI SAINI WA MAKUBALIANO YA MABORESHO YA VIWANJA VYA MICHEZO ISW

Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kimeingia makubaliano na One Tanzanite Football Academy ya kuboresha viwanja vya michezo ISW.

Makubaliano hayo yameingiwa tarehe 11 Novemba 2025 kati ya Dkt. Joyce Nyoni, Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, pamoja na Bw. Agapiti Emmanuel, Mkurugenzi Mtendaji wa One Tanzanite Football Academy. Makubaliano hayo yameshuhudiwa na timu ya Menejimenti ya Chuo cha Ustawi wa Jamii na baadhi ya maafisa kutoka One Tanzanite Football Academy.

Uboreshaji wa viwanja hivi unalenga kutoa mazingira bora kwa wanafunzi kushiriki michezo kwa usalama na kwa viwango bora, kuhamasisha mazoezi ya mwili, kukuza vipaji vya michezo, na kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika shughuli za michezo.



Wanafunzi wapya wa mwaka wa masomo 2025/2026 wakifuatilia Semina iliyotolewa katika wiki ya Usajili, Novemba 2025

## WIKI YA USAJILI WA WANAFUNZI KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), Dkt. Joyce Nyoni, aliwakaribisha wanafunzi wapya kuanza muhula mpya wa masomo mwaka 2025/2026 tarehe 21 Novemba 2025. Dkt Nyoni amewasisitiza kuwa na maadili mema, kudumisha nidhamu ndani na nje ya chuo, na kuzingatia masomo ili kufanikisha malengo yaliyowaleta chuoni. Pia amehimiza wanafunzi kutumia fursa mbalimbali zinazopatikana chuoni, ikiwemo kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii, kitaaluma, na zinazochochea ukuaji wao binafsi.

“Hamkuja tu hapa kusoma na kupata cheti cha Degree, Cheti cha Msingi, au Diploma, bali kuhakikisha mnatoka hapa chuoni mkiwa na maarifa,” alisema Dkt. Nyoni. Katika mkutano huo, Mkuu wa Chuo aliambatana na Naibu Mkuu wa Chuo Taaluma, Naibu Kaimu Mkuu wa Chuo Utawala, Wakuu wa Idara za Taaluma, Mkurugenzi wa Huduma Saidizi za Kitaaluma, Mshauri wa Wanafunzi pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo.




Zoezi la usajili wa wanafunzi wapya kwa mwaka wa masomo 2025\2026



Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni (katikati) akikabidhiwa Tuzo ya Uandaaji wa Hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu na Mhasibu Mkuu CPA Aisha Kapande (kulia) na Mkuu wa Ukaguzi wa Ndani CPA Amina Makoko (kushoto) Desemba 2025.

# ISW YASHINDA TUZO YA IPSAS MARA NANE MFULULIZO

**Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) kimeibuka mshindi wa tatu katika Tuzo za Uandaaji wa Hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma (International Public Sector Accounting Standards – IPSAS), katika kundi la Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania. Hii ni mara ya nane mfululizo tangu mwaka 2017 ambapo ISW inashika nafasi za juu kwenye mashindano haya.**

**Tuzo hizi zimetolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) usiku wa tarehe 4 Desemba 2025, katika ukumbi wa APC Bunju, jijini Dar es Salaam. Ushindi huu unaonyesha ubora wa Chuo katika masuala ya uandaaji wa hesabu za fedha.**



Naibu Mkuu wa Chuo Fedha na Utawala Dkt Zena Mabeyo (Kushoto) akipokea Tuzo ya Uandaaji wa Hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kutoka kwa Mgeni rasmi, Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Laurent Luswetula (Kulia), Desemba 2025.




Pichani ni wakufunzi wa Programu ya Uanagenzi (walioketi) pamoja na wanafunzi wa uanagenzi (waliosimama) baada ya kumalizika kwa Mkutano wa tano wa programu hiyo, uliofanyika Dar es salaam, Desemba 2025

# MKUTANO WA 5 WA WADAU NA WANAFUNZI WA UANAGENZI, WAJADILI MWELEKEO NA MAFANIKIO YA PROGRAMU YA UANAGENZI

Mkutano wa 5 wa Wadau na Wanafunzi wa Uanagenzi kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) umefanyika katika Kampasi ya Dar es Salaam, ukiwakutanisha wamiliki na wawakilishi wa taasisi mbalimbali pamoja na wanafunzi waliotarajiwa kuanza mafunzo ya vitendo kupitia programu ya uanagenzi. Mkutano huo umefanyika kuanzia tarehe 2 hadi 5 Desemba 2025.

Mkutano huo umelenga kuwajengea wanafunzi uelewa mpana kuhusu matarajio ya taasisi zinazopokea wanafunzi wa uanagenzi, taratibu za mafunzo ya vitendo, pamoja na maadili na nidhamu zinazotakiwa wakati wa utekelezaji wa programu hiyo. Aidha, wadau wamepata fursa ya kubadilishana uzoefu na chuo kuhusu namna bora ya kuwaandaa wanafunzi ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Kwa mwaka huo, programu ya uanagenzi imetimiza miaka mitano tangu kuanzishwa kwake, na imendelea kuonekana kuwa nguzo muhimu katika kuwaandaa wanafunzi kwa vitendo kupitia uzoefu wa moja kwa moja kazini. Programu hiyo imechangia kuimarisha ujuzi wa kiutendaji, kuongeza uwezo wa wanafunzi kujiajiri au kuajirika, pamoja na kupanua mtandao wao wa kitaaluma kama sehemu ya maandalizi ya kuingia katika soko la ajira.




Mkuu wa Chuo Dkt. Joyce Nyoni akihotubia katika Kongamano la Kitaaluma, Desemba 2025.




Mwezeshaji wa mada kuu Dkt. Hellen Maziko akiwasilisha mada katika kongamano la Kitaaluma, Desemba 2025.

# KONGAMANO LA KITAALUMA

**Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW), Dkt. Joyce Nyoni, amewaasa wanafunzi na wahitimu kutumia Akili Mnemba (AI) kwa weledi katika kuchakata na kuhakiki maarifa, badala ya kuhamisha moja kwa moja maudhui yanayozalishwa na teknolojia hiyo.**

**Dkt. Nyoni ametoa wito huo tarehe 18 Desemba 2025 wakati wa Mkutano wa 12 wa Kitaaluma na Maarifa, ambapo pia ametunuku vyeti kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika kozi mbalimbali chuoni hapo. Amesisitiza kuwa matumizi sahihi ya AI yanaweza kuongeza ubora wa maarifa na ubunifu wa wanafunzi endapo yatatumika kwa uadilifu wa kitaaluma.**

**Kwa upande wake, mwezeshaji wa mada kuu katika kongamano hilo, Dkt. Hellen Maziko, aliyewasilisha mada ya "Kufikiria Upya Elimu na Ajira: Akili Mnemba (AI) kama Kichocheo cha Wahitimu Walio Tayari", amesema kuwa licha ya matumizi makubwa ya AI duniani, binadamu bado ana jukumu muhimu la kufikiri, kwani AI haiwezi kuchukua nafasi ya kazi zinazohusisha maadili, hisia na ustawi wa jamii.**



Wanafunzi na wageni waalikwa wakisikiliza uwasilishwaji wa mada kuu, Desemba 2025.



Wahitimu wakisherekea katika Mahafali ya 49 (kampasi ya Dar es salaam na ya 8 (kampasi ya Kisangara) yaliyofanyika Dar es salaam, Desemba 2025.

# WAHITIMU CHUO CHA USTAWI WA JAMII WATAKIWA KUBADILI HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII KUWA BIASHARA

Wahitimu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW) wametakiwa kuwa wabunifu na kutumia elimu ya ustawi wa jamii kama fursa ya kujiajiri na kutatua changamoto zilizopo katika jamii zao.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika Mahafali ya 49 ya ISW Kampasi ya Dar es Salaam na Mahafali ya nane ya Kampasi ya Kisangara, Mkuu wa Wilaya Temeke, Sixtus Mapunda, amewahimiza wahitimu kuitumikia jamii na taifa kwa utii, uadilifu na ubunifu, akisisitiza umuhimu wa kubadilisha huduma za ustawi wa jamii kuwa fursa za kiuchumi.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Wakili Amon Mpanju, amesema wahitimu wa fani za ustawi wa jamii wana nafasi kubwa ya kusaidia jamii kutatua changamoto zao na kuboresha maisha ya wananchi.

Naye Mkuu wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Dkt. Joyce Nyoni, amesema chuo kimeanzisha programu mpya nne katika mwaka wa masomo 2025/2026 ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira. Aidha, jumla ya wahitimu 3,100 walitunukiwa vyeti katika mahafali hayo, wakiwemo wanawake 2,017 na wanaume 1,083.

# KURASA RASMI ZA CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**INSTAGRAM**
ISW_OFFICIAL_TZ

**TWITTER (X)**
TAASISIYAUSTAWI

**WHATSAPP CHANNEL**
CHUO CHA USTAWI WA JAMII

**YOUTUBE CHANNEL**
CHUOCHAUSTAWIWAJAMII

# CHUO CHA USTAWI WA JAMII

210 Shekilango Road
P.O. BOX 3375
14113 Kijitonyama
Dar es Salaam
+255735509090
+255677111200
+255716121096
or
info@isw.ac.tz